

TANGAZO

Tume ya Utumishi Serikalini inawatahadharisha Wananchi kwamba kumejitokeza baadhi ya Watu wasio waaminifu (matapeli) ambao huwapigia wananchi simu na kuwaarifu kwamba wameteuliwa kujaza nafasi za kazi na kuwataka watoe kiasi cha fedha waweze kuajiriwa katika nafasi hizo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria za Nchi, Tume inawatanabahisha waombaji kazi na wananchi kwa ujumla kwamba hakuna ajira ya Serikali inayotolewa kwa kutoa fedha.

Hivyo, Tume inawaomba wananchi kutoa taarifa za matukio hayo katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA) kupitia Nambari 113 au 0774824242.

AHSANTENI